BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 23 Februari, 2026.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

97. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kampuni ya *IRIS* inayojenga baadhi ya barabara katika kisiwa cha Pemba, imeharibu mazingira kutokana na upasuaji wa miamba, uchimbaji wa mawe pamoja na utumiaji wa *magreda* katika ardhi yenye eneo kubwa la kijiji cha Vitongoji, kuanzia Bandani Kwakoma hadi Kisiwa Njiwa.

(a) Je, kwa kiasi kipi Serikali inalifahamu tatizo hili.

(b) Ni hatua zipi zitachukuliwa kulidhibiti tatizo hili.

(c) Kwa kuwa Kampuni ya *IRIS* ndio inayoongoza kwa kuharibu mazingira hapo Vitongoji Ziwani, je, watakapomaliza watayarekebisha mazingira angalau kwa kujaza mashimo waliyoyafukua.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

45. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Naipongeza Serikali yetu kwa kuendelea kuutambua mchango mkubwa wa Maimamu wetu wa Dini ya Kiislamu na Walimu wa Madrasa, ikiwa ni pamoja na kujenga na kuhimiza maadili mema katika jamii zetu, kuhamasisha amani na utulivu wa nchi yetu, kujenga misingi ya usawa na kupunguza tofauti ya wenye wepesi na ugumu wa riziki za wananchi wetu, kwa namna Mwenyezi Mungu alivyoweka tofauti ya kipato cha waja wake.

(a) Ni lini Wizara yako itakaa pamoja na Maimamu na Walimu wa Madrasa wa jimbo la Tumbe kuwaonesha shukurani na kuwapongeza juu ya juhudi wanazozichukua katika kuitengeneza jamii yetu kimaadili.

(b) Je, Serikali imeandaa mpango gani wa kuwatambua Maimamu na Walimu wa Madrasa wa nchi nzima, taarifa za misikiti wanayosalisha na vyuo wanavyosomesha na hata kiwango chao cha elimu ya dunia na akhera.

(c) Kwa kuwa Serikali inatambua mchango mkubwa wa Maimamu na Walimu wetu wa Madrasa, ni lini itaanzisha ama kusimamia utaratibu wa Maimamu na Walimu wa Madrassa wa nchi yetu kupata mishahara au maposho ya kuwasaidia kukidhi mahitaji yao.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

15. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha usafi wa Jiji la Zanzibar, hasa katika maeneo ya mjini, pamoja na ukusanyaji taka na usafishaji wa barabara.

16. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba maeneo ya vituo vya gari na masoko yanakuwa na mazingira safi.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

69. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Ripoti mbalimbali za hivi karibuni za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zimebaini kuwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali hazina Daftari la Kuhifadhia Mali (Fixed Asset Regester). Jambo hili liko kinyume na maelekezo ya kifungu cha 29(1)(a) na (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya mwaka 2016.

Ni juhudi gani zimechukuliwa katika kuondoa au kupunguza dosari hii.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

11. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha uwekezaji katika maeneo ya kipaumbele kama vile teknolojia, nishati mbadala na miundombinu, ili kuchangia na kukuza uchumi wa Zanzibar na kuongeza ajira kwa vijana.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

236. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Miaka mingi nyuma Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanikiwa kuanzisha vyuo na skuli za ufundi kama vile Chuo cha Ufundi cha Karume (sasa KIST), skuli ya ufundi Mikunguni na Skuli ya ufundi Kengeja. Wanafunzi wengi walipita skuli hizo na kupata ujuzi mbali mbali. Hata hivyo, skuli hizo zinahitaji kupatiwa vifaa vya kisasa ili kuongeza wigo wa ujuzi kwa wanafunzi lakini zinahitaji kuongezwa fani mpya zinazoendana na wakati wa sasa na mahitaji ya aina ya uchumi tunaokwenda nao mfano mafuta na gesi.

(a) Je, hatua gani zitachukuliwa na Serikali kuwezesha vyuo na skuli za ufundi kupatiwa vifaa vipya vya kufundishia wanafunzi.

(b) Je, kuna mpango gani Serikali imeandaa kuongeza skuli na vyuo vya ufundi.

(c) Je, kuna mpango gani wa kuongeza fani mpya katika mitaala ya ufundi katika skuli za Mikunguni na Kengeja.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

23. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Serikali ina mpango gani wa kutoa mikopo nafuu kwa kina mama wanaojishughulisha na kilimo kwa kuwawezesha kununua mashine za kilimo na vifaa vya kisasa, ili kuongeza uzalishaji wenye tija katika kilimo.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

222. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Hivi karibuni Mamlaka ya Mji Mkongwe imekuwa na kampeni ya kuwaondoa wafanyabiashara za asili za Mji Mkongwe kama vile wauza kahawa, mikate ya boflo na kadhalika.

(a) Kwanini wafanyabiashara ndogo ndogo wanahangaishwa na kufukuzwa katika Mamlaka ya Mji Mkongwe.

(b) Kwanini kusiwekwe utaratibu wa kuwawezesha kufanya biashara zao za kujitafutia riziki badala ya kuwafukuza.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

141. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Serikali iliamua kuitengeneza meli ya Mv. Maendeleo kwa kuipeleka chelezoni Mombasa nchini Kenya. Katika matengenezo hayo, Serikali ilinunua *engine* za meli zikiwa mpya, lakini mwisho wake ilifanya maamuzi ya kuiuza meli hiyo na kwenda kukatwa *scraper*.

(a) Katika mauzo hayo, je Serikali iliziuza *engine* ilizozinunua zikiwa mpya.

(b) Kama hazikuuzwa, je Serikali inaweza kuwaambia wananchi kuwa zipo wapi *engine* hizo.

201. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Nane kwa kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji katika sekta ya usafirishaji wa baharini haswa Kisiwani Pemba. Kitendo hiki kimepelekea usafiri baina ya visiwa vya Pemba na Unguja kuwa rahisi mno.

(a) Je, Serikali imepata mapato ya kiasi gani kutoka mwaka 2023 hadi 2026 yanayotokana na vyombo hivyo vya usafiri.

(b) Je, ni lini Serikali itanunua boti zake zitakazorahisisha usafiri katika visiwa hivi.

(c) Je, ni lini Serikali itaanzisha huduma ya vyombo vya usafiri salama kutoka bandari ya Mkoani na kwenda katika visiwa vya pembezoni mwa jimbo la Mkoani.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

126. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMED (Jimbo la Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Mabadiliko ya matumizi ya ardhi yameongeza tishio la kupotea kwa miti ya asili na miti ya dawa kwa kasi kubwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuinusuru hali hiyo na kuihifadhi miti hiyo kwa vizazi vijavyo.

**Wizara ya Afya:**

118. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Katika Kitengo cha wagonjwa wa dharura (Emergency) cha Hospitali ya Micheweni, pamoja na huduma bora zinazotolewa, kina upungufu mkubwa wa madaktari.

Ni lini kitengo hicho muhimu sana kitaongezewa madaktari, ili kuweza kupunguza msongamano.

182. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa hivi sasa Vituo vya Afya vya Ole na Uwandani havikidhi haja ya kuwahudumia wananchi wa maeneo hayo, pamoja na kuwa ni vituo muhimu na hutegemewa na wananchi wengi wa shehia za Ole na Uwandani.

(a) Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa vituo hivyo vya afya, ili wananchi waondokane na adha wanayoipata hivi sasa.

(b) Ni upi mgawanyo wa hospitali na vituo vya afya vilivyojengwa katika majimbo ya Unguja na Pemba kwa miaka mitano ya hivi karibuni.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

41. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Nishati ya umeme ni nyezo kuu ya kuwasaidia wananchi wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba katika kukuza uchumi wao. Kwa takribani miezi mitatu sasa, kumekuwa na tatizo na usumbufu mkubwa wa kuzimwa kwa umeme mara kwa mara na kwa muda mrefu katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba bila ya taarifa yoyote kutoka kwa mamlaka inayohusika, hali inayopelekea hasara kubwa ya kiuchumi kwa wananchi wanaoitumia nishati hiyo.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea kukatika kwa nishati ya umeme mara kwa mara hapa Zanzibar.

(b) Je, ni upi mpango mkakati wa Serikali wa kuliondosha tatizo hilo ambalo limekuwa likileta hasara kubwa kwa wananchi.

(c) Kwa nini Serikali haipo tayari kufanya tathmini na kuwalipa fidia wananchi wa Zanzibar wanaopata hasara za kiuchumi kutokana na tatizo hilo linaloendelea kuwaathiri katika maisha yao ya kila siku.

62. MHESHIMIWA AZA JANUARI JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika kipindi cha hivi karibuni, kumejitokeza changamoto ya kukosekana rasilimali ya mchanga katika kisiwa cha Unguja. Hali hii imepelekea kuongezeka ugumu wa maisha kwa wananchi wetu

walio wengi ambao kipato chao kinategemea shughuli mbalimbali zinazohusiana na mchanga.

(a) Kwa kiwango gani Serikali inatambua uwepo wa changamoto hii.

(b) Ni zipi sababu zinazopelekea kuwepo kwa changamoto ya kukosekana kwa mchanga nchini.

(c) Ni lini huduma hii itarejea kama ilivyokuwa inapatikana awali.

**III. UCHAGUZI WA VIONGOZI WA UMOJA WA WAWAKILISHI WANAWAKE ZANZIBAR UWAWAZA.**

**IV. UCHAGUZI WA CHAMA CHA WABUNGE WANAWAKE WA NCHI ZA JUMUIYA YA MADOLA KADA YA ZANZIBAR (CWP).**

Zanzibar,
23 Februari, 2026.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR